




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na.14. Msimu wa Kilimo 2023/24

Tathmini ya Februari 11-20, 2024 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 21-29, 2024

MUHTASARI

- Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Masika wanashauriwa kuandaa mashamba na kupanda mazao mara tu kunapokuwa na unyevunyevu wa kutosha katika udongo huku wakipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao.
- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini hususan maeneo yanayopata mvua za Msimu zitasaidia ukuaji wa malisho na mazao
- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao na mashamba ili kuweza kukabiliana na athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza.


MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2024

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilipungua nguvu. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini zaidi na kutawala maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi.

Joto la bahari la juu ya wastani lilikuwepo katika maeneo yote ya magharibi na mashariki mwa bahari ya Hindi (pwani za Afrika Mashariki na Indonesia mtawalia). Hali hii ilikuwa na mchango hafifu katika kusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea nchini na hivyo kusababisha mifumo hafifu isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani.

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2024

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua kati ya milimita (mm) 11 hadi 150 isipokuwa maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba ambayo yalikuwa makavu kwa ujumla. Hata hivyo, maeneo machache ya mikoa ya kusini mwa Morogoro, Ruvuma, Njombe, Lindi na Mtwara yalipata jumla ya mvua kwa siku kumi kiasi cha kati ya milimita 151 na 200 kama inavyoonekana katika Kielelezo.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku 10 kwa kipindi cha Februari 11-20, 2024

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2024

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika maeneo mengi nchini hususan maeneo yanayopata mvua za Msimu zilisaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo, hali ya ukavu iliyojitokeza katika maeneo yanayopata mvua za vuli ilisaidia katika ukaushaji na uvunaji wa mazao hususan mahindi.

Maeneo yanayopata mvua za vuli, mahindi yapo katika hatua ya kukomaa na kukauka na wakulima wameendelea na uvunaji wa zao hilo na pia waliendelea na kuandaa mashamba kwa ajili ya kupanda mazao ya msimu wa Masika. Hata hivyo, wakulima katika maeneo yanayozunguka ziwa victoria waliendelea na upandaji wa mahindi na maharage.

Mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu hususan katika mkoa wa Njombe yapo katika hatua ya ukuaji wakati viazi mviringo vipo katika hatua ya kukomaa. Hata hivyo, katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Dodoma mahindi yapo katika hatua ya kubeba wakati katika

Na.14. Msimu wa Kilimo 2023/24

mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma, na Rukwa mahindi yapo katika hatua ya kubumba. Wakulima wengi katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka waliendelea na shuguli za palizi, uwekaji mbolea na madawa ya kuua wadudu.

Zao la pamba katika mkoa wa Tabora hususan katika Wilaya ya Uyui limeathirika kutokana na hali ya mvua ya muda mrefu katika maeneo hayo.

Kwa maeneo yanayolima mpunga hususan katika mikoa ya Tabora, Mbeya, Rukwa na Morogoro baadhi ya wakulima waliendelea na shughuli za kupandikiza mpunga kwenye vijaruba na kwa waliowahi kupanda mpunga upo katika hatua ya ukuaji na wakulima wameendelea na palizi.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama umeendelea kuimarika nchini.

HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 11-20, 2024

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde kimeendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-29, 2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kubakia maeneo ya kusini zaidi mwa nchini.

Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea kuwepo katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuendelea kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi, hali hii inatarajiwa kuchangia katika kusafirisha hewa yenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika baadhi ya maeneo nchini hasa yale yaliyopo mashariki hususan katika kipindi cha nusu ya pili ya dekad.

HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-29,2024

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi hadi za wastani vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika nusu ya pili ya dekad.

Tathmini ya Februari 11-20, 2024 na Matazamio kwa Kipindi cha Februari 21-29, 2024

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) zinataraajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache hususan katika kipindi cha nusu ya pili ya dekad.

HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-29, 2024

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitasaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo ambao utasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao hususan kwa maeneo yanayopata mvua za Msimu. Hata hivyo, mvua hizo zikiwa nyingi zinaweza kuathiri ukuaji wa mazao hayo.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Masika wanashauriwa kuendelea na shughuli za uvunaji mahindi na maharage na pia kuandaa mashamba na kupanda mazao mara tu kunapokuwa na unyevunyevu wa kutosha katika udongo huku wakipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao.

Katika maeneo yanayopata mvua za Msimu, wakulima wanashauriwa kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na unyevunyevu wa udongo wa kupitiliza, kutuama kwa maji kwa mashamba yaliyoko mabondeni, na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza.

Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki, na kuchukua tahadhari kwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi ili kuepuka athari zitokanazo na upepo mkali na mvua kubwa pale vinapojitokeza.

Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya kutosha na kuchimba mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-29,2024

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye.